European Journal of
Linguistics
(EJL)

# Tathmini ya Nyimbo za Kiswahili Kama Nyenzo ya Ufundishaji Katika Shule za Chekechea



CARI Journals

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 3, pp 1 - 18, 2025
www.carijournals.org

# Tathmini ya Nyimbo za Kiswahili Kama Nyenzo ya Ufundishaji Katika Shule za Chekechea

[1*]**Pius M Mwanza,**[2]**Dkt Sarah Ngesu,**[3]**Dkt F. M. Musyoka**

[1,2,3]South Eastern Kenya University

https://orcid.org/0009-0001-6073-8539

*Accepted: 4th June,2025, Received in Revised Form:4th July,2025, Published: 4th August, 2025*

## Ikisiri

**Lengo la Utafiti:**Utafiti huu ulinuia kutathmini nyimbo za Kiswahili zinazotumika katika shule za chekechea kama nyenzo ya ufundishaji katika kata nne za Kaunti ya Makueni ambazo ni Mukaa, Kilungu, Kathonzweni na Makueni. Madhumuni ya utafiti huu ilikuwa ni;Mosi, kuainisha aina za nyimbo za Kiswahili zilizotumika kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za chekechea nchini Kenya.Pili, kubainisha namna nyimbo za Kiswahili zilivyotumika kama nyenzo ya ufundishaji.Tatu, kufafanua athari za matumizi ya nyimbo za Kiswahili kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za chekechea.

**Mbinu za Utafiti:**Kaunti ya Makueni ina idadi ya kata tisa kwa ujumla. Kata hizi nne ziliteuliwa kwa sababu utafiti wa awali ulionyesha kwamba kwenye kata hizo kuna shule za chekechea ambazo zina mchanganyiko wa walimu na wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini Kenya na waliozungumza lugha asili tofauti.Shule saba za kiserikali na tatu za kibinafsi ambazo zenye wanafunzi wengi zilishughulikiwa katika utafiti huu. Shule mbili hadi tatu zilichaguliwa katika kila kata kulingana na idadi ya wanafunzi na maeneo ya shule hizo.Mbinu ya kusudio ilitumika kuchagua nyimbo za Kiswahili ishirini na tano kwa jumla. Sampuli lengwa ilikuwa ni shule saba za kiserikali na tatu za kibinafsi. Pia, mbinu ya hojaji ilitumika katika ukusanyaji wa data kutoka kwa walimu.Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa kutumia njia ya kimaelezo na kitakwimu.Utafiti uliongozwa na nadharia ya kiutambuzi iliyoasisiwa na Jean Piaget mwaka wa 1954.

**Matokeo ya Utafiti:**Utafiti huu umebaini kwamba nyimbo za Kiswahili ni mojawapo ya nyenzo muhimu ya ufundishaji katika shule za chekechea nchini Kenya.

**Mchango wa Kipekee kwa Nadharia, Sera na Mazoezi:**Kwa Nadharia:Utafiti uliongozwa na nadharia ya kiutambuzi iliyoasisiwa na Jean Piaget mwaka wa 1954.Kwa Sera:Nyimbo za Kiswahili zilitumika katika ufundishaji katika sehemu kubwa kwa kuwa zilieleweka na wanafunzi wote.Kwa Mazoezi:Nyimbo za Kiswahili zinazotumika katika shule za chekechea kama nyenzo ya ufundishaji.

**Maneno ya Kimsingi:** *Nyimbo za Kiswahili, Nyenzo za Ufundishaji, Shule za Chekechea*

## Utangulizi

Katika karatasi hii, tutashughulika na nyimbo za Kiswahili zinazotumika kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za chekechea nchini Kenya. Lengo hili liliongozwa na madhumuni mahususi, ‘‘Kufafanua namna nyimbo za Kiswahili zinatumika kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za chekechea nchini Kenya?’’ Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti, “Ni kwa namna gani nyimbo za Kiswahili zinazotumika kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za chekechea nchini Kenya.” Katika utafiti huu, tatizo lilikuwa ni kutathmini nyimbo za Kiswahili zinazotumika katika shule za chekechea kama nyenzo ya ufundishaji huku tukiegemea sana namna zinavyotumika.Nyimbo za watoto wa shule za chekechea huwa na upekee wake ukilinganisha na zile zingine. Huwa zina mafunzo kwa watoto hawa yanayoenda sambamba na silabasi ya elimu nchini. Tukiangalia kwa mfano, somo la hesabu, utatambua kwamba msingi wake ndio wanasoma kupitia kwa nyimbo hizo. Wakati wamalizapo kiwango hiki cha elimu ikiwa ni kipindi cha miaka miwili, huwa na msingi kamilifu wa kupambana na kiwango kifuatacho cha elimu ambacho ni shule ya msingi. Inakuwa hivyo katika masomo yale mengine ambayo yanasomeshwa katika shule za msingi. Utafiti wetu uliafiki kwamba nyimbo hizi ni mojawapo wa mbinu zitumikapo kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za chekechea nchini Kenya. Upekee mwingine wa nyimbo hizi ni kwamba namna nyimbo hizi zinaundwa, zinakuwa na lugha rahisi na zinapotumiwa kwa watoto hawa, wanazielewa kwa urahisi na pia, zinazingatia kiwango cha umri wao. Tena, sio refu sana na zina uwezo wa kuchukua akili zao. Hali hii inawafanya kuwa na jambo la kufanya kila siku.Wataalamu wengi wa lugha ya Kiswahili wameshughulikia swala hili la nyimbo za Kiswahili ingawa hawakuegemea sana upande huu wa watoto. Wametafiti tu nyimbo za jumla ambazo nyingi zinahusika na watu wazima na shule za kiwango cha juu kuanzia shule za msingi. Hili kudhibitisha ukweli wa kauli hii, tutaangalia mifano ya wataalamu hawa na nyimbo zao.

## Namna  Nyimbo Zilivyoshughilikiwa na Watafiti Mbalimbali

Wataalamu wengi wamebobea katika nyimbo za lugha ya Kiswahili. Tunapochunguza nyimbo zao, nyingi zimehusika na mambo ya watu wazima. Tutaangalia mifano ya kazi zao bila kuingilia kwa undani sana.Baadhi ya kazi hizi ni kama; mtaalamu Mutwiri (2005) aliyeshughulika na nyiso za tohara za jamii ya Watigania kwa kuzingatia mtazamo kuhusu utendakazi wa nyimbo za kiasili. Alikuwa na lengo la kuonyesha umuhimu wa nyimbo za tohara katika jamii ya Watigania na kueleza sababu za tamaduni hizi kutokufa isipokuwa upinzani ulikuwa ni mwingi sana. Nyimbo hizi twatambua zilikuwa muhimu katika jamii hii ya Watigania kwa kuwa ziliwafunza mambo kadha wa kadha na kuwezesha utamaduni wao kuendelea.Mtafiti mwingine aliyeshughulikia nyimbo ni Mwaniki (2011). Alifanya utafiti wake kuhusu matumizi ya lugha katika nyimbo tohozi za Salim Junior. Aliweza kuchanganua nyimbo ambazo Salim Junior alizitoa lengo likiwa kuonyesha jinsi Salim Junior alivyotohoa nyimbo za wasanii wengine.Hadijah (2013) alichunguza mafunzo ya nyimbo za jandoni na unyago kwa jamii ya Wahiya tarafa ya Lulindi. Utafiti ulichunguza ubora na udhaifu wa mafunzo hayo kwa jamii

hiyo.Mburu (2014) ni mtafiti mwingine aliyetalii fani katika nyimbo za Anastacia Mkabwa. Lengo lake lilikuwa kuchunguza matumizi ya fani katika nyimbo za injili hasa kwa kumrejelea mtunzi Anastacia Mkabwa.Mtaalamu mwingine aliyeshughulika na nyimbo ni Ramadhan (2017). Aliangalia dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto katika jamii ya Makunduchi. Malengo makuu yalikuwa ni kuchunguza dhamira za nyimbo za kubembeleza za watoto mifano kutoka Makunduchi. Mtaalamu huyu ni baadhi ya wale wachache waliotafiti kazi ya watoto.Umi (2018) alichanganua maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo. Nyimbo za msondo kulingana na mtafiti katika jamii ya Wadigo ni aina ya nyimbo ambazo huimbwa wakati wa harusi na jamaa wa bibi.Kurgat (2019) naye alifanya utafiti kuhusu usemezano katika amani miongoni mwa jamii tatu teule za Kenya. Nyimbo alizoshughulikia ni zile zilizoimbwa baada ya uchaguzi wa kitaifa. Nyimbo alizotafiti ni zile zilizoimbwa baada ya ghasia zilizoshuhudiwa nchini Kenya baada ya uchaguzi wa kitaifa uliofanywa mwaka wa 2007. Azima kubwa ya utafiti huu ilikuwa kubainisha sifa za usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii za Wakipsingisi, Wakisii na Waluo.Utafiti mwingine ulioshughulika na nyimbo ni wake Aaron na mwenzake (2021). Utafiti huu ulijikita katika athari za kimaadili zitokanazo na nyimbo za muziki wa Singeli nchini Tanzania. Kilichomfanya afanye utafiti wa nyimbo za Singeli ni kupitia madai kwamba nyimbo zake zilichangia kuporomoka kwa maadili ya jamii. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba nyimbo hizo za Singei ziliakisi uhalisia wa matendo adilifu pamoja na matendo yasiyo adilifu yaliyotendeka katika jamii ya Waswahili wa Tanzania.Mwisho ni utafiti wake Hamad, (2022) aliyefanya kuhusu kuchunguza dhamira na matumizi ya lugha katika nyimbo za ngoma ya msewe wa Kambini Kichokochwe mkoa wa kasikazini Pemba. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kutumia kigezo cha dhima, nyimbo za ngoma ya msewe wa Kambini Kichokochwe mkoa wa kasikazini Pemba zinaweza kuwekwa katika makundi ya nyimbo za siasa, nyimbo zinazokuza umoja na ushikamano, nyimbo za kusifu, kukejeli, nyimbo zinazokuza utamaduni, nyimbo zinazofichua maofu, nyimbo za maadili na nyimbo zinazoonya jamii. Mtafiti aliyekaribia kufanya kazi inayokaribiana na yetu ni Mbabazi (2023). Alitafiti kuhusu matumizi ya nyimbo katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Madhumuni yake yalikuwa namna nyimbo zinavyoweza kutumiwa darasani katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Hapa mtafiti hakutumia nyimbo za Kiswahili kama nyenzo za ufundishaji kama tulivyofanya lakini kupitia kwa kazi yake, twatambua kuna ulinganifu wa kiasi.Waandishi tulioangalia kazi zao hapo juu walishughulikia nyimbo kwa ujumla isipokuwa wale wachache tuliowaona. Kazi hii imedhihirisha ya kwamba kuna pengo lililoachwa la kushughulikia watoto wa shule za chekechea ambao ndio tulitafiti.

**Nadharia**

Nadharia iliyoongoza kazi hii ni yake Jean Piaget (1896 – 1980) ambayo ni nadharia ya kiutambuzi. Iliasisiwa mwaka wa 1954. Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kutangamana na matini husika kwa lengo la uelewaji wa hatua za mwanzo wa funzo. Nadharia ya Jean Piaget ya maendeleo ya utambuzi ilitambulisha kwamba watoto huenda hatua nne katika maendeleo ya

akili. Nadharia hii inalenga tu sio kuelewa jinsi watoto wanapata ujuzi lakini pia kuelewa asili ya akili. Hatua zenyewe ni;

i) Hatua ya fikra za jaha: kuzaliwa hadi miaka miwili. Katika hatua hii watoto wanapata ujuzi kupitia uzoefu wa kimwili na usimamizi wa vitu vya jirani.
ii) Kipindi cha ujumuisha wa dhana; umri wa miaka miwili hadi miaka saba.Katika hatua hii ya pili, watoto watajua ulimwengu kupitia mchezo.Hata hivyo kwa mchakato wa mchezo rahisi wa nje, kuna mchakato mgumu wa ujuzi wa mantiki na mtazamo wa wengine.
iii) Matendo halisi; umri wa miaka saba hadi miaka kumi na moja. Katika hatua hii , watoto wameanza kufikiri kimantiki zaidi lakini mawazo yao bado hayana mabadiliko kwa kufikiria kama watu wazima.Wao kama sheria, hawaelewi na huzichukua dhana za kufikiri.
iv) Kazi ya uendeshaji rasmi; umri wa miaka kumi na mbili na

Kazi hii ililenga watoto wa shule za chekechea walio na umri kati ya miaka miwili hadi saba. Kwa hivyo hatua ya kiwango hiki ni ya pili.

**Namna Nyimbo Zilijumlishwa**

Tuliweza kujumulisha nyimbo katika makundi sita kulingana na maudhui ya kila mojawapo. Mifano ni kama ifuatayo;

i) Kidini
ii) kiulimwengu
iii) kiushauri
iv) kuburudisha
v) kuonya
vi) mafunzo mengineyo

**Jedwali lifuatalo litaweza kudhihirisha haya kupitia kwa utafiti wetu.**

| Aina za Nyimbo | Wanaotumia | | Wasiotumia | |
|---|---|---|---|---|
| Dini | 36 | 90% | 4 | 10% |
| Kiulimwengu | 35 | 87.5% | 5 | 12.5% |
| Kushauri | 33 | 82.5% | 7 | 17.5% |
| Kuburudisha | 35 | 87.5% | 5 | 12.5% |
| Kuonya | 33 | 82.5% | 7 | 17.5% |
| Mafunzo Mengineyo | 38 | 95% | 2 | 5% |

Jedwali hili linaonyesha jinsi nyimbo zilivyojumlishwa kulingana na maudhui ya kila kikundi. Yale watoto hawa wanasoma kupitia kwa nyimbo hizo yanakuwa msingi wa wanachoenda kukumbana nacho wanapoingia katika kiwango cha shule za juu kuanzia shule za msingi. Kufuatana na utafiti wetu, tunaona kwamba kiwango cha matumizi ya nyimbo hizo shuleni kiliachana kwa asilimia ndogo sana. Nyimbo za mafunzo mengine ndizo zilitumiwa na walimu wengi ambao walikuwa 38 ikiwa ni asilimia 95. Zilifuatwa kwa karibu sana na zile za dini zilizotumiwa na idadi ya walimu 36 ikiwa ni asilimia 90. Nyimbo za kiulimwengu na za kuburudisha zilitumika kwa kiwango kimoja na walimu 35 ikiwa ni asilimia 87.5. Mwisho ni nyimbo za kuonya na za kushauri zilizotumiwa kwa kiwango kimoja cha walimu 33 ikiwa ni asilimia 82.5. Nyimbo kadhaa zilihifadhiwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya utafiti.

**Ufafanuzi Wa Namna Nyimbo za Kiswahili Zinavyotumika kama Mbinu za Kufundisha Katika Shule za Chekechea**

Sehemu hii inaonesha jinsi nyimbo zilizokusanywa zinavyotumika kama nyenzo ya kufundishia. Utafiti umebainisha kwamba nyimbo zinatumika kufundishia maudhui za aina mbalimbali kama inavyodhihirishwa katika sehemu ndogondogo zifuatazo.

**Kufundishia Chemsha Bongo**

Matokeo yanaonesha kwamba baadhi ya nyimbo zinatumika kama chemsha bongo kwa lengo la kuchochea fikra za wanafunzi. Watoto huimba nyimbo hizo, wakiwa wamechangamka kupitia vitendo vinavyoambatana na uimbaji wa nyimbo husika. Nyimbo hizo huwa hazina maudhui au mafunzo muhimu kwa watoto bali hutekeleza kazi ya kuchemsha bongo kama maandalizi ya kufuatilia somo linalotarajiwa kwa siku hiyo. Nyimbo hizo zinakuwa na sehemu muhimu ya kutekeleza kazi hiyo ya kuwachangamsha wajifunzaji. Ufuatao ni mfano wa wimbo wa chemsha bongo:

*“Mabata madogo dogo x2*

*Yanaogelea x2 katika shamba nzuri la mti wa juu (yanafanya kwakwa*

*Kwakwa x2) Katika shamba*

*Nzuri la mti wa juu x 2”*

Katika wimbo huu, sehemu ya kuchangamsha bongo ni;

*“yanafanya kwakwa kwakwa x2.*”

Hapa mabata ndio hufanya hivyo na watoto hufanya vitendo hivi wakijilinganisha na mabata wakiwa wanafurahia maji. Wimbo mwingine ambao ni kwa ajili ya kuchemsha bongo ni huu ufuatao:

*“(Maua x2, na ni nani maua) x2*

*Turuke kidogo na tukatike kidogo x2”*

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 3, pp 1 - 18, 2025
www.carijournals.org

Katika wimbo huu, sehemu inayowakilisha hoja hii ni; *“turuke kidogo na tukatike kidogo x2”*. Watoto wanapofikia sehemu hii ya wimbo, huruka na kutikisa viuno wakifurahia na kuchangamsha akili zao kwa ajili ya kupokea maudhui ya somo la siku hiyo. Pia katika wimbo mwingine:

*“(Umbi umbi) aumbi*

*(Umbi kanyama) aumbi*

*(ahuui) chakacha*

*(Piga gita) gita*

*(songa nywele) nywele*

*(zungusha marinda) marinda.“*

unawachangamsha watoto hawa katika kifungu kifuatacho;

*“( ahuui ) chacha. (Piga gita) gita. (Songa nywele) nywele. (Zungusha marinda) marinda.”*

Wimbo na. 14 ambao ni;

*“(Watoto wadogo njooni tucheze)*

*Watoto wadogo njooni tucheze*

*(Tutacheza na kuimba) tutacheza na kuimba*

*(Tutaimba na kucheza) tutaimba na kucheza*

*(Tucheze pamoja) tucheze pamoja).“*

Unachangamsha watoto hawa katika kwa mfano katika kifungu kifuatacho:

*“(Tutacheza na kuimba)“ tutacheza na kuimba. (Tutaimba na kucheza) tutaimba na kucheza. ( Tucheze pamoja) tucheze pamoja.”*

Kuhusiana na aina hiyo ya maudhui, mfano wa mwisho ni wimbo nambari 15 wenye maneno yafuatayo:

*“(Agoya goya) Agoya*

*(Agoya goya) Agoya*

*(Na tanu wetu) Agoya*

*(Tafuta wako) Agoya*

*(Tingisha naye mandiamba) Huu...*

*(Tingisha naye mandiamba) Huu...”*

Ambapo kifungu kinachochangamsha watoto hawa chapatikana katika sehemu ifuatayo;

*(Tingisha naye mandiamba) huu. (Tingisha naye mandiamba) huu*

Ni muhimu kutambua kwamba watoto kutokana na umri wao hawakuwa na njia nyingine ya kujifurahisha wakiwa shuleni isipokuwa kupitia nyimbo za hiyo. Umri wao hauwawezeshi kuwa na lugha ya majadliano na ndio sababu wakati hawakuwa na la kufanya, wanatulia kama wagonjwa. Nyimbo hizi zinawafurahisha na kucheka huku wakiwa na utulivu wa kisaikolojia kwa ajili ya kufuatilia somo lililoandaliwa kwa siku hiyo. Walimu walitoa mchango mkubwa walipokuwa wakiziimba nyimbo hizo kwa sababu walihusika katika uimbaji pamoja na wanafunzi moja kwa moja. Kwa hivyo, nyimbo za Kiswahili ni muhimu katika kiwango cha elimu ya awali na hasa zikitumiwa kama nyenzo ya ufundishaji katika elimu ya awali.

**Kufundishwa Rasilimali za Nyumbani**

Baadhi ya nyimbo zilitumika kuwafundisha wanafunzi rasilimali za nyumbani. Ni muhimu watoto kutambua umuhimu wa rasilimali zitumikazo katika jamii zao ili kuweza kuzitunza na kuzitumia kwa namna inayofaa. Mifano ya rasilimali hizo ni pamoja na maji na miti. Katika wimbo ufuatao wanaimba :

*"Maji ni maisha x2*

*Hatuwezi kuishi bila maji. Tunaosha nayo, tunapika nayo, tunakunywa maji ;*

*Hatuwezi kuishi bila majix2."*

Wimbo huu unaeleza juu ya maji ambayo kulingana na wimbo ni maisha. Unaendelea kueleza kwamba hatuwezi kuishi bila maji. Pia, maji hutumika kwa kunywa ili kuendeleza maisha. Mtoto akifahamu mambo hayo hukua akijua kwamba maji ni muhimu maishani mwake na kila wakati atayatunza. Wimbo mwingine uliimbwa kama ifuatavyo:

*"Miti ni muhimu x2*

*Hatuwezi kuishi bila miti x2*

*Tuna chanja kuni, tunapika nayo, hatuwezi kuishi bila kuni x2."*

Lengo la wimbo huo ni kufundisha watoto umuhimu wa miti katika maisha ya binadamu. Unaeleza jinsi miti ilivyo na maana maishani. Miti hutumiwa kama kuni katika kupika chakula; kwa hivyo bila miti, hatuwezi tukapata kuni za kupikia chakula.Njia inayofaa ya kuwafunza watoto kwa kila mojawapo ni kupitia nyimbo kwa kuwa mwalimu huonesha mifano ya vitu hivyo wakati wanapokuwa wakiimba. Pia, huwaeleza umuhimu wa kila moja ya vitu hivyo katika maisha yao ya kila siku. Hali hii huwawezesha kuelwa kabisa kile walichofunzwa.

**Kufundishia Dini**

Matokeo yanaonesha kwamba baadhi ya nyimbo zilitumika kufundishia dini. Ni muhimu watoto kutambua kuwa kuna Mungu mwenye uwezo wa kutupatia uhai, kututunza na kutuzuia kuepukana na shida zozote za ulimwengu. Ingawa dhana ya Mungu haina ithibati ya kisayansi

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 3, pp 1 - 18, 2025
www.carijournals.org

lakini mapokeo ya hifu ya Mungu yana mchango mkubwa katika malezi ya watoto hivyo hayawezi kupuuzwa.

*Mtoto Yesu x2*

*Nakupenda x2*

*Wewe ni mwokozi wa kila siku x2."*

Wimbo huo unaelezea juu ya mtoto Yesu na kwamba wanapaswa kumpenda. Yeye ndiye mwokozi wa kila siku katika maisha tunayoishi. Kupitia kwa maelezo haya wanaopata kupitia kwa wimbo huu, watoto hawa watakua wakimheshimu huyu Yesu. Pia, huu ni utangulizi wa somo la dini ambayo wanapatana nayo katika shule za msingi na kuendelea.Kulingana na Wikipedia, Kamusi Huru, nyimbo za kidini zinafafanuliwa kuwa chanzo cha nguvu na njia ya kupunguza maumivu, kuboresha hali ya mtu na kusaidia katika ugunduzi wa maana katika mateso yake. Ni muhimu kutambua ni kupitia kwa kuimba watoto wa shule za chekechea hupata mafunzo ya neno la Mungu kwa kuwa umri wake haumruhusu ufunzwaji wa kawaida.

**Kufundishwa Herufi**

Matokeo yanaonesha zaidi kwamba baadhi ya nyimbo kutumika kama nyenzo ya kufundishia herufi. Mtoto wa kiwango cha shule za chekechea huanza kwa kufunzwa herufi hizo ambazo ni a, e, i, o, u. Huu ndio msingi wa kujifunza kusoma na kuandika kwa sababu tunatumia herufi hizo katika kuandika maneno. Nyimbo hizo mbili ni wimbo namba 5:

*"Tusome Kiswahili lugha yetu*

*lugha tamu a e i o u x2."*

na wimbo na. 19 ambao ni;

*"a e i o u*

*Hizi ni herufi tu*

*Zatoa sauti tu tamka kwa sauti tu*

*A – angalia*

*E – Enda*

*I - ingia*

*O – Ondoka*

*U – Usiende "*

Kuna njia nyingi za kufunza watoto ambao hawajui kuandika na hawana lugha yoyote ya mawasiliano; uimbaji ukiwa mojawapo. Huziimba nyimbo hizi wakikariri herufi hizo mpaka wanazifahamu kabisa. Mwalimu hufanya kazi nyingi hili kuona kila mtoto amejua herufi hizi kabisa.

Kufundishwa Hesabu

Baadhi ya nyimbo zilitumika katika kufundishia hesabu. Nyimbo hizo zimeundwa kwa njia ya kipekee hili kuwezesha mtoto kuzifahamu kwa urahisi. Wimbo namba 6 ambao unaimbwa kwa maneno yafuatayo:

*“Hapa pana moja na moja hapa mchezo gani huu kanyanga x2*

*Hapa pana mbili na mbili hapa mchezo gani huu kanyanga x2.”*

Wimbo huu umeundwa kama wa kucheza ambapo nambari moja imewekwa mahali mtoto anapaswa kuikanyanga wakati unapofika kufanya hivyo. Pia, nambari mbili imewekwa hivyohivyo. Wanapomaliza kuimba baada ya kurudia wimbo mara kadhaa, kila mtoto anakuwa ameelewa nambari hizo. Wimbo namba.8 unaendeleza maudhui hayo kama unavyoonekana hapa chini:

*“Hapa pana moja na moja ni mchezo wa paka na panya x2.”*

Wimbo huu unafunza watoto jinsi ya kuandika nambari moja na mbili. Ingawa wimbo umeundwa kama mchezo, ilikuwa ni mbinu tu yakuwawezesha kuelewa zaidi nambari hizi. Walizikanyanga huku wakipewa jina la paka na wengine panya. Wimbo na.16 ni;

*“(Chungwa moja) peremende*

*(Chungwa mbili) peremende*

*(Chungwa tatu) peremende*

*(Chungwa nne) peremende*

*(Chungwa tano) peremende*

*(Chungwa sita) peremende*

*(Chungwa saba) peremende*

*(Chungwa nane) peremende*

*(Chungwa tisa) peremende*

*(Chungwa kumi) peremende*

*(Haya twende) x2 weka mtoto chini.“*

Wimbo huu unaanza kwa kuzungumzia chungwa na peremende vikiwa ni vitu wanavyovifahamu na hata kuzipenda. Wanaanza na chungwa moja kila mmoja akionyesha mpaka chungwa la kumi. Wimbo unaofuata ni wa na.18 ambao ni;

*“Maskini punda alinyimwa pembe*

*Akapewa masikio ati ndio pembe x2*

*Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa tunajua kusoma.”*

Wimbo unaanza na mnyama punda vile alinyimwa pembe akapewa masikio. Utangulizi huu unawaleta karibu na kile wanaenda kusoma ambalo ni nambari moja hadi tisa. Wanarudia mara kadhaa mpaka wanaelewa kuzikariri. Wimbo na. 20 nao ni;

*"Mama mdogo yule ameketi pale x2*

*Anafunza mtoto wake kusoma x2*

*Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa kumi ndio mwisho."*

Wimbo wenyewe unaanza kwa kuonyesha mama anayefunza mtoto wake kusoma. Hali huwa ni la kawaida huko nyumbani na kwa hivyo inamfanya mtoto awe makini anaposoma nambari hizi. Hapo wanaanza kuimba kuanzia nambari moja hadi kumi. Tunapoangalia wimbo unaofuata ni wa na.21 ambao ni ;

*"Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa tumefika kumi.*

Wimbo huu unaanza moja kwa moja kuanzia nambari moja hadi kumi. Hii ni kwa sababu wamezikariri nambari hizi mpaka wakazielewa. Wakati wanamalizia shule za chekechea baada ya miaka miwili, huwa wanazifahamu nambari hizi zote.Nyimbo hizi hufunza watoto hawa herufi hizi ukiwa ndio utangulizi wa somo la Hesabu. Somo hili ni baadhi ya masomo yaliyo muhimu katika elimu yetu hapa nchini na hata duniani kwa jumla. Mwalimu huandika nambari hizi na kuwaonyesha mifano yote wanapoendelea na kuimba. Baadaye, huwapa kila mmoja herufi moja na wakati inapotajwa, mtoto anainua lile lake kudhihirisha ameifahamu. Kila mmoja huwa na wakati wake wa kurudia hayo.Walimu hawa hutia bidii sana mpaka kila mtoto anakuwa na uwezo wa kuzikariri na kuziandika herufi zote za hesabu kabla ya kufuka kiwango kingine cha elimu.

**Kufundiswa Viwango vya Watu Katika Jamii**

Wimbo uliowakilisha sehemu hii ni wimbo nambari saba ( 7) ambao ni;

*Mwalimu x2, mtu muhimu sana*

*Mungu twakuomba tulindie mwalimu*

*Baba x2, Mama x2, Dada x2, Kaka x2, Nyanya x2, Babu x2*

*Mtu muhimu sana*

*Mungu twakuomba*

*Tulindie wazazi"*

Wimbo huu ndio unawakilisha aina za nyimbo hizi. Unaanza na mwalimu akionyeshwa kama mtu muhimu katika jamii na kumuombea hiili Mungu amlinde. Anayefuata mwalimu ni baba na wale wengine wameorodheshwa kama ifuatavyo; mama, dada, kaka, nyanya, babu. Mtoto hukua akielewa vile hawa watu katika jamii ni muhimu na jinsi wanahitajika kupewa heshima. Umuhimu wa watoto kujua viwango hivi vya watu katika jamii zetu ni kumwezesha kutambua

kila mtu na heshima zake. Shule za chekechea huwa ndio mojawapo ya msingi muhimu wa kufunza watoto hawa yale yote yaliyohitajika katika jamii. Kwa hivyo wakielekezwa kutambua huyu ni nani katika jamii na heshima zake, watakua wakijua hayo siku za usoni. Hali hii inawasaidia kuwa na heshima kwa watu wazima wanapoendelea na kukua wakiwa katika jamii.

**Kufundishia Sayansi**

Nyimbo zilizowakilisha sehemu hii ni wimbo nambari 9, 10, 11 na 23. Nyimbo hizi zinaeleza mahali wanyama hawa wanamoishi na kile wanachokula. Mifano ya wanyama hawa ni kama vile samaki, ndege na paka. Wimbo na. 9 ni mfano wa wimbo huu ambao ni;

*"Maua ya shambani yanamea na ndege wa angani wanaruka na mimi*

*Na wewe tufurahie mwokozi.*

*Watoto wadogo njooni tucheze x2*

*Tucheze na kusoma tusome pamoja."*

Wimbo unafunza watoto juu ya mahali ndege hutoa chakula chao ambapo ni kwa maua yanayomea shambani. Wimbo huu unafunza pia vile ndege hawa huruka angani nao wanafurahia maumbile ya Mungu. Mfano mwingine ni wimbo na. 10 ambao ni;

*"Samaki mnyama mdogo, huishi ndani ya maji*

*Akiona mwanadamu, huzama ndani ya maji,*

*Samaki mnyama mdogo, Samaki ni chakula x2."*

Wimbo huu unaelezea kuhusu samaki ambao ni wanyama wanoishi majini na ni chakula cha binadamu. Wimbo na. 11 ni mfano mwingine ambao ni;

*"Paka, paka, paka, unataka nini?*

*Nataka maziwa, pesa ziko wapi?*

*Ziko kwa mfuko, mfuko huko wapi?*

*Nimeusahau wewe paka x4, miaw x4."*

Wimbo huu unazungumza juu ya mnyama paka ambaye hukunywa maziwa na hutoa sauti ya *miaw"*. Wimbo wa mwisho ni na. 23 ambao ni;

*Nyumbani kwetu ii u x2*

*Kuna mbuzi mee x2*

*Kuna ng'ombe moo x2*

*Kuna mbwa wuu x2*

*Kuna paka miaw x2*

*Kuna kuku kwea x2*

*Kuna punda oioi x2*

Wimbo huu unaofunza watoto hawa baadhi ya wanyama wanaoishi nyumbani wakiwa ni; mbuzi, ng'ombe, mbwa, paka, kuku na punda. Nyimbo zote zinaonyesha kila mnyama na sauti anayotoa. Watoto waliimba wakitoa sauti hizo huku wakifurahia sana. Nyimbo hizo zinawakilisha msingi wa somo la Sayansi. Kwa hivyo huu ni utangulizi muhimu wa kufunzwa masomo ya kisayansi wakiwa katika umri mdogo. Ni muhimu kutambua nyimbo hufanya kazi kubwa katika kuweka msingi wa maisha kwa watoto hawa wa shule za chekechea.

**Kufundishwa Maadili**

Nyimbo hizi ziliwakilishwa na wimbo nambari 17. Nyimbo za aina hii ni muhimu kwa watoto kwa sababu zinajaribu kuweka msingi wa maisha yao katika siku zijazo. Watoto wanakua wakiwa na tabia njema jambo ambalo ni muhimu katika jamii. Wimbo wenyewe wa na.17 ni;

*"Napenda mambo yoote ya shule kabisaa X2*

*Najifunza kusoma x2*

*Na pia kuandika x2*

*Soma soma soma wee x2*

*Mtoto wa mwalimu soma wee x2*

*Ndani ya kitabuu soma wee x2*

*Katika ubao soma wee x2."*

Wimbo huu unamshauri mtoto vile anahitajika kupenda mambo yote ya shule. Wimbo unaelezea mambo hayo ambayo ni kama kusoma kwa ubao, kusoma vitabu na hata kuandika. Mtoto anapoendelea na kuimba wimbo huu, huendelea kuyaweka mambo hayo akilini akijua kwamba mambo hayo ndiyo muhimu anayohitaji kuyatilia bidii hili kufaulu maishani. Akipanda ngazi za juu kielimu, hatacheza na mashauri hayo aliyoyapata akiwa mchanga. Ni jambo muhimu kwa kila mtu kutambua ushauri huleta wokovu maishani mwake, kwa familia, kwa jamii na kwa viongozi mbalimbali. Kupitia kwa biblia katika kitabu cha Mithali 11: 14, inasema kwamba, "Pasipo mashauri, taifa uanguka; bali kwa wingi wa washauri huja wokovu." Walimu huchukua nafasi ya kuwaelezea watoto maana ya kila wimbo baada ya kuimba. Hali hii huwasaidia kuelewa zaidi wimbo wenye ushauri. Kulingana na maelezo hayo, ni wazi kabisa njia iliyokuwa muhimu kuwafunza mashauri ni kupitia uimbaji wa nyimbo za Kiswahili zilizotumika kama nyenzo ya ufundishaji.

**Kufundishwa Aina za Vyakula**

Mfano wa nyimbo za aina hii unawakilishwa na wimbo nambari 22 ambao ni;

*"Chapati mkate wa mbofulo*

*Ni chakula kizuri cha kutupa nguvu."*

Wimbo unaelezea aina ya vyakula tunavyovitumia nyumbani kama vile chapati na mkate wa bofulo. Pia, unaelezea umuhimu wa vyakula hivi katika mili yetu kwamba vinatupatia nguvu tunapovila. Wimbo huu ukiwa ni mfano wa nyingi wanazoziimba, unawawezesha kukua wakijua maana zaidi ya kila chakula mwilini jambo ambalo ni muhimu sana. Nyimbo hizi ni msingi wa somo la *Home Science* ambayo hipo katika mtaala wa masomo yetu nchini. Wakati walipokuwa wakiimba, mwalimu aliwaonyesha mifano ya vyakula hivyo. Hali hii iliwasaidia kutosahau na kufahamu zaidi aina ya vyakula hivyo.

**Kufundishwa nyakati Maalum**

Nyimbo za aina hii huonyesha kukamilika kwa kipindi fulani na mwanzo wa kingine katika siku. Mfano wa nyimbo za aina hii unawakilishwa na wimbo nambari 24 ambao ni;

*"Nasikia sauti x2*

*Sauti ya mama x2*

*Sasa ni saa sita x2*

*Mwalimu kwa heri x2*

*Watoto kwa heri."*

Wimbo ulianza na ishara ya mama kupitia kwa sauti. Unasema, *"sasa ni saa sita, mwalimu kwa heri, watoto kwa heri".* Mara hiyo, kila mtoto tulimwona akikimbia akienda nyumbani huku anaendelea kuimba kwa sauti ya juu. Huu ni mfano wa wimbo unaodhihirisha kumalizika kwa kipindi cha shule na kuanza kwa kipindi kingine cha kuelekea nyumbani. Nyimbo za aina hii husaidia watoto kutambua mabadiliko ya wakati kwa sababu hawawezi kuelewa kusoma saa za kawaida ambapo wale wa kiwango cha juu hutumia kengele. Hawangeweza kufahamu saa ya kawaida hata ikiwa ukutani lakini wimbo uliwawezesha kuelewa mabadiliko ya wakati wa siku kupitia kuimba kwao. Mwalimu kazi yake ilikuwa wakati wa kipindi fulani ukifika, alikuwa anaanzisha wimbo unaowasilisha kipindi hicho nao wakizingatia hayo. Kwa hivyo, wakati wa kipindi cha masomo ukiisha, mwalimu alianza kuimba na watoto wote wakimfuata wakiimba huku wakielekea nyumbani jambo ambalo walikuwa wameizoea. Hali hii ni muhimu kwa mtoto kwa sababu atakapopanda viwango vya juu kielimu kama shule za msingi, atakuwa na uwezo wa kuzingatia nyakati hizi. Kupitia kwa hayo yote, mtoto alifunzwa kupitia nyimbo za Kiswahili zilizotumika kama nyenzo ya ufundishaji. Kufundishia Bembelezi.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 3, pp 1 - 18, 2025
www.carijournals.org

Mfano wa nyimbo za bembelezi ulipatikana katika wimbo nambari 25 ambao ni;

*"Lala mtoto lala x2*

*anakuja lala x2*

*Akupe maziwa mama lala x2."*

Nyimbo bembelezi ni nyimbo zinazoimbiwa watoto watulie, waache kulia na walale. Hakuna njia nyingine ya kutuliza watoto hawa isipokuwa kuwanyonyesha lakini wakati wazazi hawakuweko nyumbani, watoto walipoachiwa watoto wale wadogo, walitumia nyimbo hizi kuwatulize hasa walipolia. Baada ya kuwaimbia, walinyamaza na hata kulala. Nyimbo hizi pia ziliwaburudisha watoto hawa wachanga walipoimbiwa. Mtoto aliweza kuimbia ndugu yake mdogo akimzungusha na pia kumbembeleza mpaka anakimya na kulala. Nyimbo bembelezi huimbwa kwa utaratibu na kwa sauti nyororo kama tulivyoshuhudia wakati wa utafiti. Sauti nyororo huchukua umakinifu wa mtoto katika hali yake ya kusikiza. Huwa pia anaburudika wakati anapoimbiwa. Pia, sauti nyororo husababisha mazingira ya mtoto kuingia kwa ulimwengu wa kulala.Nyimbo ni muhimu katika jamii zetu za Afrika kwa jumla. Watoto wanahitaji kufunzwa wakiwa wachanga kwa sababu nyakati nyingi ndio huachiwa ndugu na dada zao wachanga wakati mama wameenda katika shughuli zingine za boma. Walimu waliwafunza nyimbo hizo huku wakiwaonyesha mifano kupitia kwa wenzao.

**Hitimisho**

Ni muhimu kutambua kuwa nyimbo hizi zinafaa kutumiwa kama nyenzo ya Ufundishaji katika shule za Chekechea nchini Kenya. Zikiunganishwa na mbinu zingine za Kufundishwa, matokeo yanakuwa ya kufana. Tunatambua Kila kikundi Cha nyimbo kinakuwa na maudhui tofauti na kile kingine lakini kwa ujumla, zinaendeleleza Yale husomwa katika kiwango kifuatacho Cha elimu ambacho ni shule za msingi.

**Mapendekezo**

Utafiti umebaini kwamba kiwango hiki cha elimu hakijaingiliwa sana na wasomi na waandishi wengi. Kwa hivyo twapendekeza uwanja huu uweze kuingiliwa zaidi. Pia, Kila mwalimu anahitajika kutumia nyimbo za Kiswahili kama nyenzo ya Ufundishaji katika shule hizi za chekechea wanapofunza darasani. Shule nyingi zilikuwa na mwalimu mmoja ambaye hangeweza kufanya vizuri kwa sababu alihitaji wakati wa kujitayarisha kabla ya kuandaa somo darasani. Tulipendekeza Kila shule ya chekechea iwe na walimu wawili na zaidi kulingana na kiwango cha watoto. Tena, semina na warsha zaidi ziandaliwe kuwafunza walimu hawa hili kufahamu yanayojiri Kila kukicha.

**Marejeleo**

Abdulrahim, H. T. A. (2014). Taashira na Utendaji katika Nyimbo za Harusi za Waswahili wa Unguja. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Egerton.

Ahereza, P. (2023). Dhima ya Nyenzo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule za Upili katika Munispaali ya Kabale. Tasnifu ya Shahada ya Sanaa, Chuo Kikuu cha Kabale,

Akivaga, S. K. na Odaga, A.b. (1982). *Oral Literature*. A School CertificateCourse. Nairobi: Heinemann.

Angushi, M. E. (2019). Mchango wa Tamasha za Muziki katika Ufundishaji wa Uanishaji wa Nyimbo katika Shule za Upili Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabii.

Brown, J. (1993). *Audio Visual Instruction Techniques, Media and Methods*. MC Graw – Hill, Inc.

Chiuri, J. (1984). Pop Music as a form of Oral Literature: A Survey of Joseph Kamaru.Tasnifu ya P.G.D.E. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Creswell, J. W. (2012). *Educational Research: Planning, Conducting and Evaluating Qualitative and Quantitative Research*. Boston: Pearson.

Cross, G.P. (1974). *The Psychology of Learning*. Paris: Pergamon Press.

Dales, E. (1999). *Audio visual methods in Teaching*. New York: Holt Renehalt, and Winston, inc.

Ellis, R. (1999). The Empirical Evaluation of Language Teaching Material: ELT Journal Vol 5, No.1PP 112-119.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Flanders, N. A. (1970). *Analyzing Teaching Behaviour*. New York: Addison- Wesley Co.

Gage, N. (2009). *Educational Psychology*; Chicago Rand and Nally Education.

Idrissa, S. M. (2014). Mchango wa Nyimbo za Ngoma ya Mdatu katika Kudumisha Maadili ya Jamii ya Watu wa Mafia. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Iyaya, R. M., Nabea R.W. na Mayaka J.G. (2021). Mtindo na Lugha ya Uwasilishaji katika Nyimbo za Jando za Jamii ya Watachoni kutoka Kenya, Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya. Toleo Cons. J. Kiswahili, 2 (1), 231-253.

Hadija, U.R. (2013). Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa Jamii ya Wahiyao Tarafa ya Lulindi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Huria, Tanzania.

Haji, Z. R. (2017). Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo Bembelezi za Watoto: mfano katika Makunduchi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Hamad, B. A. (2022). Kuchunguza Dhamira na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Ngoma ya Msewe wa Kmbini Kichokochwe, mkoa wa Kaskazini Pemba. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria.

Hegel, G. W. (1975). *Aesthetics*. New York: Oxford University Press.

Joachim, M. K. (2019). Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi: mfano wa Shule za Upili za Kaunti ndogo ya Moiben, Kenya. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabii.

Juma, M. K. (2019). Upimaji wa Ufahamu wa Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia Shule za Msingi: mifano kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.

Kamau, H. W. (2015). Tathmini ya Matumizi ya Vifaa vya Kufundisha Msamiati wa Kiswahili katika Shule za Msingi za Umma, Kaunti ya Kisumu Mashariki, Kenya.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kariuki, P.M. (2017). Matumizi ya Nyenzo katika Ufunzaji wa Kiswahili katika Shule za Msingi za Umma Jimbo la Nyandarua, Kenya.Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kassim, B., M`raiji, J.and Manasseh, L. (2020). Aina ya Nyenzo katikaUfundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari Nchini Kenya. V. 2( 2),143- 152.

Kevogo, A. U. na Kandagor, M. (2022). Kiswahili kama Nyenzo ya Kufundishia Elimu ya Uraia katika Taasisi za Elimu Nchini Kenya. *Jarida ya CHAKAMA*, 1, 81-90.

Kieti, M. na P. Coughlin. (1970). *Barking, you will be eaten! The Wisdom of Kamba Literature*. Nairobi: Phoenix.

KimondiO, D. K. (2019). Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Sifo Wakamba. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Machakos.

Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi.* Shungwaya Publishers. Nairobi.

Kombo, D. T. and Tromp.D. L. A. (2006). *Proposal Thesis Writing: Introduction.* Nairobi: Paulines Publication Africa.

Kothari, C.R. na Garg. G. (2016). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Third Edition. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kurgat, (2019). Usemezano katika Nyimbo za Amani miongoni mwa Jamii Tatu teule za Kenya. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kabianga.

Liambila, N. M. (2010). *Uchunguzi wa Matumizi ya Kiswahili katika Ufunzaji na Ujifunzaji wa Shule za Chekechea katika Manispaa ya Webuye, Wilaya ya Bungoma, Kenya*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlni Press.

Marolyne, J. M. (2019). Uchanganuzi wa Kisemantiki-Leksia wa Maneno Teule ya Kiswahili yaliyotumika katika Nyimbo Teule zilizoimbwa na Nonini na Juacali. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno.

Mbabazi. A. (2023). Matumizi ya Nyimbo katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili. Makerere University, Kampala, Uganda.

Mburu, J. M. (2014). Fani katika Nyimbo za Anastacia Mukabwa, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. UDSM Journals, https:// Journals. Udsm, ac.tz.

Miruka, O. (1994). *Encounter with Oral Literature.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mukandabvute, A. A. na Gores, M. (2021). Athari za Kimaadili zitokanazo na Nyimbo za Muziki wa Singeli Nchini Tanzania.

Musembi, N.N. (2016). Mabadiliko ya Maudhui katika Nyimbo za Jando: Mfano kutoka Jamii ya Wakamba.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

Mutegi, L. (2010). Maigizo katika Fasihi Simulizi mfano wa Kirarire katika Nyimbo za Tohara za Wameru.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso katika Jamii ya Watigania.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwaka, M. W. (2016). Dhima za Nyimbo za Sengo katika Uzini Zanzibar. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Huria, Tanzania.

Mwaniki, M. W. (2011). Matumizi ya Lugha katika Nyimbo Tohozi za Salim Junior. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nandwa, J. na Bukenya.A.(1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longmann.

Ntarangwi, M. (1990). Uhakiki wa Maudhui ya Utetezi katika Utunzi wa Remmy Ongola.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Neema, S. N. (2023). Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania: Uchunguzi Kifani Wilaya ya Temeke. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, cha Tanzania.

Ngesu, S. N. M. (2021). Tafsiri katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni Nchini Uganda. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Odera, F. Y. (2010). *School Radio Programmes; A case study of its use in selected institutions in Nyanza region in Kenya*. MPH (Thesis Wales Great Britain).

Ojode, J. O. (2017). Uchanganuzi Kiplagmatiki wa Sitiari katika Nyimbo za Taarab: mfano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally, Unguja.

Okello, Z.A., Kirimi J. & Ong'ang'a H.O. (2022). Public Pre-Primary School Teachers' Use of Play as a Classroom Teaching Strategy: A Case of Bunyala, Busia County, Kenya. *Journal of Research Innovation and Implication in Education*, 6 (1),359-369.

Okeyo, L. A. Kimemia J. N. na Ndethiu, S. M. (2023). Uchunguzi wa Mielekeo ya Walimu na Wanafunzi kuhusu Mbinu na Nyenzo za Kufundishia katika Shule za Upili za Umma, Kaunti za Kisumu na Kakamega, Kenya. *East Africa Journal of Swahili Studies 6(1): 435 – 454.*

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature.* Indiana. Uiversity, Bloomington.

Okwalo, P.O. (2012). Matumizi ya Nyenzo katika Ufundishaji wa Fashi Simulizi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari Wilayani Mumias na Matugu.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Riziki, O. N. (2016). Mchango wa Nyimbo za Michezo ya Watoto katika Kukuza Maadili ya Jamii ya Wapemba. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania.

Robinson, A. (1980). *Principals and Practices of Teaching*. London; George Allenand Unwin.

Sjoerdsma, S. (2016). *Importance of Play: Play- Based Insrtruction within a Preschool Learning Enviroment.* Dordt College

Suleimani, A. H. (1998). *Media Audio – Visual. Pengajara*: PT Gramedia.

Tumaini, S. M. (2022). Nafasi ya Nyimbo katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili kwa Watoto wa Elimu ya Awali. Mulika, Na. 41 (2), 242 – 262. Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswhili. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Umi, S. K. (2018). Uchanganuzi wa Maudhui ya Nyimbo za Msondo na Athari zake kwa Wanandoa katika Jamii ya Wadigo. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Pwani.

Vygotsky, L. S. (1978). *Mind in Society: The Development of Higher Psychological Processes*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Wamitila, K. M. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wanyenya, W. (2020). Maudhui katika Nyimbo za Tohara za Wamasaaba Nchini Uganda. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Makerere.

Wray, A. na Bloomer, A. (2006). *Project in Linguistics, A Practical Guide to Researching Language*. London: Hodder Education.

Zacharia, U. (2012). *Maandalizi ya Ufundishaji*. Dar es Salaam: Luwingu Wordpress.

Zaharia, M. A. (2018). Taathira za Ubabedume kwa Mwanamme Mwenza wa Kizanzibari kupitia Nyimbo za Taarab Asilia. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Zanzibar (Suza).

©2025 by the Authors. This Article is an open access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/)